## HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI MDOGO WA HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA TAREHE 08/01/2022

**MAHUDHURIO**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | LUSAJO | MWALUKASA | MWENYEKITI |
| 2 | TENSON | MKASIWA | KATIBU |
| 3 | JULIUS | SHULLA | MJUMBE |
| 4 | WILSONI | MTAFYA | MJUMBE |
| 5 | VICTOR | MAGAFU | MJUMBE |
| 6 | ABDUL | SALIM | MJUMBE |
| 7 | NEEMA | BUKUKU | SEKRETARIET |

**WAJUMBE WAALIKWA**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | TIMOTHEO | MASSAWA | MWANASHERIA |
| 2. | DICKSON | KISENIME | MHANDISI |

**AGENDA ZA KIKAO**

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO
3. KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA
4. KUPOKEA NA KUJADILI MIRADI ILIYOPATA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA KUTOA RIDHAA MATUMIZI YA NJIA YA ***FORCE ACCOUNT*** KATIKA KUTEKELEZA MIRADI HIYO KWA MWAKA HUSIKA
5. MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI
6. KUFUNGA KIKAO

**AGENDA NA. TTC/CTB/3.07.2021/01: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao, Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 4:18 asubuhi mara baada ya kuridhika na mahudhurio ya wajumbe. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na kuwataka kuwa watulivu ili tuweze kujadili kwa usahihi agenda zilizopo mbele yetu.

**AGENDA NA. TTC/CTB/3.07.2021/02: KURIDHIA AGENDA ZA KIKAO**

Mwenyekiti alimtaka katibu kusoma agenda zote za kikao ili ziweze kusikika kwa wajumbe na kasha wato maoni yao kama wanaridhia agenda husika. Katibu alisoma agenda zote kama zilivyoorodheshwa kwenye kabrasha kasha mwenyekiti aliwahoji wajumbe kama wanaridhia agenda wajumbe wote kwa kauli moja waliridhia agenda za kikao.Hivyo mwenyekiti alimtaka Katibu kusoma agenda inayofuata.

**AGENDA NA. TTC/CTB/3.07.2021/03 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA.**

Katibu alisimama na kusoma muhtasari wa kikao cha robo kilichopita na kasha mwenyekiti aliruhusu wajumbe tupitie ukurasa kwa ukurasa muhtasari husika ili kujiridhisha na kilichoandikwa. Hivyo wajumbe walipitia ukurasa kwa ukurasa na kujiridhisha na Pia wajumbe walitoa baadhi ya marekebisho ambayo yanahitajika kufanyika. Baada ya kupitia muhtasari huo wajumbe walipitisha na kuthibitisha pamoja na marekebisho yake.

**AGENDA NA. TTC/CTB/3.07.2021/04 KUPOKEA NA KUJADILI MIRADI ILIYOPATA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 NA KUTOA RIDHAA MATUMIZI YA NJIA YA *FORCE ACCOUNT* KATIKA KUTEKELEZA MIRADI HIYO KWA MWAKA HUSIKA.**

Mwenyekiti alimtaka katibu Kuwasilisha orodha ya miradi inayotarajia kupata fedha kutoka serikali Kuu ambayo pia utekelezaji wake unaanza mwaka huu wa fedha mara baada ya kupokea fedha kutoka Serikali Kuu. Katibu alisimama na kuwasilisha miradi hiyo kama ifuatavyo;

| Na | JINA LA MRADI UNATARAJIWA KUTEKELEZWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 | IDARA HUSIKA | BAJETI TENGWA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Hospitali ya Mji Tunduma Katika Kata ya Mpemba awamu ya 6 | AFYA TIBA | 1,000,000,000 |
| 2 | Ununuzi wa Vifaa 4 vya Kituo cha Afya katika Hospitali ya Mji Tunduma | AFYA TIBA | 500,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa Nyumba 1 ya Mkurugenzi | UTAWALA | 150,000,000 |
| 4 | Ujenzi wa Jengo la Utawala awamu ya Pili (Phase II). | UTAWALA | 1,000,000,000 |
| 5 | Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Mpemba | FEDHA NA BIASHARA | 600,000,000 |
| 6 | Ujenzi wa Hostel 1 katika eneo la | | 304,000,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | maegesho ya malori ya magari makubwa | FEDHA NA BIASHARA | |
| 7 | Ujenzi wa Mgahawa (Canteen) Eneo la maegesho ya magari makubwa | FEDHA NA BIASHARA | 96,000,000 |
| 8 | Umaliziaji wa Zahanati 2 zilizoanzishwa na jamii katika kata ya Chipaka na Niumba-Chiwezi | AFYA TIBA | 100,000,000 |
| 9 | Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa kwa Shule za Msingi | ELIMU MSINGI | 112,500,000 |
| 10 | Umaliaziaji wa vyumba vya madarasa na maabara kwa shule za Sekondari | ELIMU SEKONDARI | 250,000,000 |
| 11. | Ujenzi wa jengo la Idara ya Dharura (EMD) | IDARA YA AFYA | 300,000,000 |
| 12 | Ujenzi wa Nyumba ya watumishi (3 in 1) | IDARA YA AFYA | 90,000,000 |
| 13 | Ujenzi wa soko la Machinga | IDARA YA FEDHA | 300,000,000 |

Baada ya uwasilishaji huo, katibu alisema kuwa kwa mwaka huu wa fedha tunaonza Julai mosi Halmashauri inatarajia kupokea fedha hizo kutoka Serikali Kuuili tuweze kutekeleza miradi iliyopo kwenye bajeti hasa miradi hiyo mikubwa inayotegemea fedha kutoka serikali Kuu.

Mjumbe mmoja akasema fedha hizo bado hazijafika ila tunatarajia kufika mara baada ya kuwasilisha nyaraka za kuombea fedha katika Ofisi ya Rais TAMISEMI, hivyo tunategemea fedha hizo zikifika tuanze utekelezaji mara moja.

Katibu, alitoa ushauri kuwa tunahitaji kutoa Matangazo kwa ajili ya kuwaalika watoa huduma ili wawee kuomba kazi hizo za Ujenzi kwa miradi hii iliyotengewa fedha kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Pia akatoa ufafanuzi kuwa "tumependekeza kuwa tuanze na Taasisi za Umma katika kuzishindanisha, na tukiona Taasisi za Umma zimeweka makadirio ya juu (bei kubwa) tunaalika makampuni binafsi ili nayo tuone gharama zao katika utekelezaji wa mradi".

Mwenyekiti, alisema "ni njia ipi ya kimanunuzia mbayo tunaweza kutumia katika kutekeleza miradi hiyo" Mjumbe mwingine akajibu kuwa kwa miradi mingi ya Serikali inatekelezwa kwa njia ya **Force account**, hivyo hatuwezi kuikwepa katika kutekeleza miradi katika Halmashauri.

Mwanasheria, alishauri kwamba ni vizuri tukatumia njia ya manunuzi ya force account katika kutekeleza mradi huu kuliko kutumia wakandarasi.

Mhandisi wa ujenzi alisema gharama zinajulikana **force account** ni nzuri na inaokoa gharama ukilinganisha na wakandarasi, pia Mhandisi alieleza kuwa "wakandarasi huwa wanaongeza Overhead Cost na VAT katika gharama zao.

**Maamuzi ya Kikao;** Wajumbe wote kwa kauli moja waliridhia kutumia njia ya Force Account katika utekelezaji wa miradi tajwa hapo juu pindi tu utekelezaji wake utakapoanza mara baada ya kupokea fedha kutoka Serikali Kuu

**AGENDA NA. TTC/CTB/3.07.2020/05: MENGINEYO**
Hapakuwa na mengineyo

**AGENDA TTC/CTB/3.07.2020/06: KUFUNGA KIKAO**
Katibu alimkaribisha mwenyekiti kufunga kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango na ushiriki wao kwenye kikao na kuwatakia kazi njema.Hatimaye mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 8:40 Mchana.

**IMESAINIWA LEO TAREHE.........**

| | |
|---|---|
| ............................ | ........................ |
| LUSAJO MWALUKASA | TENSON MKASIWA |
| **MWENYEKITI** | **KATIBU** |